

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MADINI

Telegramu "MADINI".  
Simu: + 255-26 2320051  
Nukushi : +255 26 2322282  
Baruapepe : ps@madini.go.tz



Mji wa Serikali,  
S. L. P. 422  
**DODOMA**

**6 Agosti, 2019**

**TAARIFA ILIYPOCHAPISHWA NA MTANDAO WA  
VOANEWS/REUTERS KUHUSU UTOAJI WA LESENI MBILI  
KUBWA (SML) REFINERIES NA SMELTERS**

Tarehe 24 Julai, 2019, saa 17:33 Mtandao wa Voanews ulichapisha taarifa yenye kichwa cha habari: **Chinese Firms to Build Gold Smelter, Refineries in Tanzania**, iliyoandikwa na Kampuni kubwa ya habari duniani ya Reuters.

Taarifa hiyo ilitaja chanzo cha habari kuwa ni hotuba ya Waziri wa Madini, Mhe. Doto Biteko aliyotoa tarehe 24 Julai, 2019 Ikulu Jijini Dar es salaam wakati wa hafla fupi ya kupokea na kukabidhiwa dhahabu ya Tanzania iliyokamatwa nchini Kenya.

Sehemu ya taarifa iliyochapishwa na mtandao huo kwa lugha ya Kiingereza kwa tafsiri ya Kiswahili ilimnukuu Waziri Biteko akieleza kwamba;

***Tanzania imetoa leseni za ujenzi wa Mitambo ya uchenjuaji madini, moja ya kuchenjulia kwa njia ya kuyeyusha (Smelter) na ya pili ya Mitambo miwili ya kuchenjulia dhahabu kwa njia ya kusafisha (refinery) kwa makampuni ya China kama sehemu ya jitihada za serikali kukusanya mapato kupitia sekta ya madini.***

Aidha, taarifa iliyofanana kama hiyo ilichapishwa katika gazeti la The Guardian la hapa nchini la tarehe 26 Julai, 2019, lenye kichwa cha Habari **“Government Silent on Chinese venture in gold smelting, refinery plant”**.

Gazeti hili pia lilieleza kuhusu kutolewa kwa leseni hizo bila kutaja jina la kampuni wala nchi zinakotokea kampuni hizo. Katika maelezo ya gazeti hilo, linaeleza kuwa, katika mahojiano baina ya The Guardian na Waziri limemnukuu kuwa, Waziri alipotakiwa kutaja jina la kampuni alisema hawezi kusema chochote.

Wizara ya Madini inapenda kutoa ufafanuzi kuwa, katika hafla hiyo, ambapo Waziri wa Madini, Mhe. Doto Biteko alipewa fursa na Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kuzungumza alieleza ifuatavyo;

**“Nataka nikuhakikishie Mhe. Rais, kwenye historia ya nchi hii katika sekta madini, kwa mara ya kwanza toka mwaka 2010 hatujawahi kutoa leseni ya uchimbaji wa madini yenye gharama kubwa yaani, *Special Mining Licences (SML)* ambayo uwekezaji wake ni dola milioni mia moja (USD 100m). Katika kipindi chako Mhe. Rais, tunazo leseni mbili tutazitoa”**.

**“Nafurahi kukuambia Mhe. Rais tayari tumekwisha kutoa leseni mbili za Refinery kwa ajili ya dhahabu lakini tumetoa leseni moja kwa ajili ya kutengeneza smelter”, alisema Waziri.**

Katika hotuba yake, Waziri Biteko hakutamka leseni hizo zimetolewa au zitatolewa kwa kampuni gani, ya nchi gani, majina yake au taarifa zake. Vilevile, alichokieleza Waziri ni mchakato wa kuzipata kampuni zitakazowekeza kwenye Refinery na Smelter ambapo alieleza kwamba, wizara ilipokea maombi 37 ambayo yalichambuliwa kwa kusikiliza kampuni moja baada ya nyingine na kila kampuni ilifanya uwasilishaji (presentation) lengo likiwa ni kuangalia uwezo wa kifedha na historia ya kila kampuni.

Hivyo, kutokana na alichokizungumza Waziri katika hotuba yake, hakuna alipotamka jina la nchi wala kampuni zitakazopewa au zilizopewa leseni hizo.

Imetolewa na;

Asteria Muhozya  
**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Kny: KATIBU MKUU**